

04- Kuwajibika Hajj

Hajj ni nguzo ya tano kwa Waislamu. Maamrisho yake yametajwa katika Qur-aan na Sunnah, Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

وَلِلّٰهِ عَلٰى النّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلٰيْهِ سَبِيلًاٰ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللّٰهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ١٧

((Na kwa ajili ya Allaah ni wajibu kwa watu watekeleze Hajj katika Nyumba hiyo kwa mwenye uwezo. Na atakayekanusha, basi hakika Allaah ni Ghaniyy (Mkwasi) kwa walimwengu))¹

Nguzo zote tano za Kiislaam zimetajwa katika Hadiyth ifuatayo:

عَنْ أَبْنَى عُمَرَ (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا): قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ((بُنْيَ الْإِسْلَامُ عَلَى خَمْسٍ، شَهَادَةٍ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ وَإِقَامُ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءُ الزَّكَاةِ وَاحْجُجْ وَصَوْمُ رَمَضَانَ))

Imepokelewa toka kwa Ibn ‘Umar (رضي الله عنهم) kwamba: Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ((*Uislamu umejengwa kwa [nguzo] tano; Kushuhudia kwamba hapana ilaah (muabudiwa wa haki) isipokuwa Allaah, na kwamba Muhammad ni Rasuli wa Allaah, na kusimamisha Swalaah, Kutoa Zakaah, kuhiji na kufunga Swawm Ramadhwaan*))²

Na katika Hadiyth ndefu maarufu ya Jibrily (عليه السلام) alipomfikia Rasuli (صلى الله) kufundisha mambo ya Dini ya Kiislamu...

((أَنْ تَشْهَدَ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَتَقِيمَ الصَّلَاةَ وَتُؤْتِيَ الزَّكَاةَ وَتَصُومَ رَمَضَانَ وَتَحْجُجَ الْبَيْتَ إِنْ اسْتَطَعْتَ إِلٰيْهِ سَبِيلًا))

((...*Ushuhudie kwamba hapana ilaah (mwabudiwa Anayestahiki kuabudiwa kwa haki) isipokuwa Allaah, na kwamba Muhammad ni Rasuli wa Allaah, na usimamishe Swalaah, utoe Zakaah, ufunge Swawm ya Ramadhwaan na uhiji ukiwa na uwezo*))³

¹ Aal-‘Imraan (3: 97).

² Al-Bukhaariy na Muslim.

³ Muslim.

Limekuwa ni jukumu kwetu, bali ni haki ya Allaah (سبحانه وتعالى) tunayopaswa kuitimiza kama Aayah hiyo inavyodhihirisha. Asiyeitimiza haki hii ya Allaah (سبحانه وتعالى) hali ya kuwa na uwezo, atakuwa amekanusha amri hiyo, na atakuwa hakutimiza Uislamu wake. Hapo itakuwa ni khasara kwake kwa vile manufaa ya 'ibaadah zote yanamrudia mtu mwenye kwa sababu Allaah (سبحانه وتعالى) Hanufaiki na chochote katika 'ibaadah zetu bali bin Adam ndiye mwenye kupata manufaa na ni wenyewe kumhitaji Allaah (سبحانه وتعالى).

Allaah (سبحانه وتعالى), Hakuiwajibisha nguzo hii kutekelezwa zaidi ya mara moja katika uhai wa mtu. Juu ya hivyo, kuitekeleza kwake iwe kwa mwenye uwezo tu. Hii ni Rahmah ya Allaah (سبحانه وتعالى) kwa waja Wake kutokuwafanyia ugumu katika Dini hii tukufu. Rasuli (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliitekeleza nguzo hii mara moja tu katika uhai wake na aliamrisha hivyo kama ilivyo katika Hadiyth ifuatayo:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) قَالَ: خَطَبَنَا رَسُولُ اللَّهِ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) فَقَالَ: ((أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ فَرَضَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ الْحَجَّ فَحُجُّوا)) فَقَالَ رَجُلٌ: أَكُلَّ عَامٍ يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ فَسَكَتَ حَتَّىٰ قَاتَلَهَا ثَلَاثًا فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ): ((لَوْ قُلْتُ نَعَمْ لَوْ جَبَتْ وَلَمَا اسْتَطَعْتُمْ ثُمَّ قَالَ: ذَرُونِي مَا تَرَكْتُكُمْ فَإِنَّمَا هَلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ بِكَثْرَةِ سُوَالِهِمْ، وَاحْتِلَافِهِمْ عَلَىٰ أَنْبِيائِهِمْ فِإِذَا أَمْرَتُكُمْ بِشَيْءٍ فَأَتُوْا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَإِذَا نَهَيْتُكُمْ عَنْ شَيْءٍ فَدَعُوهُ))

Kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) amesema: "Rasuli wa Allaah (صلی الله علیہ وسلم) alitukhutubia akasema: (**(Enyi watu Allaah Amekufaridhisheni Hajj hivyo mhiji)**). Mtu mmoja akasema: Kila mwaka ee Mjumbe wa Allaah? Akanyamaza kimya hadi yule mtu aliporudia mara tatu [swali lake] akasema Rasuli wa Allaah (صلی الله علیہ وسلم): (**((Ningelisema ndio, ingeliwajibika, na wala msingeliweza))**). Kisha akasema: (**((Niacheni kwa yale niliyokuachieni kwani watu wa kabla yenu waliangamia kwa maswali yao mengi na ikhitilaaf zao [kujadiliana sana kwoo] na Mitume yao. Hivyo nnapokuamrishi jambo lifanyeni muwezavyo na ninapokukatazeni jambo jiepusheni nalo))**)⁴

⁴ Muslim.

Hakuna ubaya kwa mwenye uwezo kutekeleza zaidi ya mara moja kwa ajili ya kupata fadhila zaidi kutokana na dalili zifuatazo:

عن ابن عباسٍ (رضي الله عنهم) أَنَّ الْأَقْرَعَ بْنَ حَابِسٍ سَأَلَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ الْحَجُّ فِي كُلِّ سَنَةٍ أَوْ مَرَّةً وَاحِدَةً؟ قَالَ: ((بَلْ مَرَّةً وَاحِدَةً، فَمَنْ زَادَ فَهُوَ تَطْوِعٌ)) رواه أبو داود وصححه الألباني

Kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهم) kwamba Al-Aqra' bin Haabis alimuuliza Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) : "Ee Rasuli wa Allaah, je, Hajj ni kila mwaka au mara moja tu?" Akasema: (**(Ni mara moja lakini mwenye kupenda kuzidisha ni tatwawwu')**) [kujitolea na anapata ujira wake].⁵

عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ (رضي الله عنه) أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((قَالَ اللَّهُ: إِنَّ عَبْدًا صَحَّحْتُ لَهُ جَسْمَهُ، وَوَسَعْتُ عَلَيْهِ فِي الْمَعِيشَةِ يَكْضِي عَلَيْهِ خَمْسَةُ أَعْوَامٍ لَا يَفْدُ إِلَيَّ لَمْحُرُومٌ))

Kutoka kwa Abu Sa'iyd Al-Khudriyy (رضي الله عنه) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: (**((Allaah Amesema: Hakika Nikimpa siha mja mwilini na nikampa uwezo wa maisha, ikampitia miaka mitano asiye Kwangu [Kuhijji] ameharamishwa))**).⁶

Uwezo na masharti ya kuwajibika mtu kutekeleza nguzo hii:

1. Muislamu.
2. Huru (asiye mtumwa).
3. Aliyebaleghe.
4. Mwenye akili timamu.
5. Mwenye uwezo wa mali, asiwe na deni la mtu isipokuwa deni linaloendelea kulipwa.
6. Mwenye uwezo wa kiafya, ikiwa hali inamruhusu kusafiri bila ya kuathiri afya yake au kuhatarisha maisha yake. Mfano wa atakayehatarisha uhai wake ni mgonjwa ambaye mafigo yake hayafanyi kazi na anahitaji kusafishwa kila baada ya siku moja au mbili.

⁵ Abu Daawud ikasahihishwa na Al-Albaaniy.

⁶ Ibn Hibban katika Swahiyh yake, Abu Ya'laa, 2/304; Al-Bayhaqiy, 5/262.

7. Mahram – kwa mwanamke.
8. Kuwe na amani na usalama wa kufika Makkah.

Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa

- Vijana kutokutekeleza nguzo hii kwa kungojea hadi wafike umri mkubwa. Hili ni kosa kubwa kwani hakuna ajuaye kama ataishi hadi afikie umri mkubwa. Na ametuonya Rasuli (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ):

((مَنْ أَرَادَ الْحُجَّ فَلِيَتَعَجَّلْ)) رواه الإمام أحمد وأبو داود وابن ماجه. وفي رواية أحمد وابن ماجه:
((فَإِنَّهُ قَدْ يَمْرُضُ الْمَرِيضُ، وَتَغْرِبُ الْحَاجَةُ)) حسنة الألباني في صحيح ابن ماجه.

((Mwenye kutaka kufanya Hajj basi aharakishe))⁷ Na katika riwaaya ya Ahmad na Ibn Maajah – **((Kwani huenda akapata maradhi au akafikwa na haja))**

Vile vile amesema Rasuli (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ):

((تَعَجَّلُوا إِلَى الْحُجَّ) (يعني الفريضة) فَإِنَّ أَحَدَكُمْ لَا يَدْرِي مَا يُعْرَضُ لَهُ)) أخرجه الإمام أحمد
رحمه الله وحسنه الألباني في إرواء الغليل.

((Harakizeni [kuteketeleza] Hajj, kwani hajui mmoja wenu nini kitamsibu))⁸

- Kutokana na Hadiyth zinazodhihirisha kuhiji kila baada ya miaka mitano, baadhi ya watu wanadhania kwamba imewajibika hivyo. Wanachuoni wamekubaliana kwamba dalili hizo hazimaanishi kwamba Hajj imewajibika kila baada ya miaka mitano, bali ni 'Mustahabb' (inapendekeze ka) kwa sababu ni vyema kuwapa fursa Waislamu wengineo wasiokuwa na uwezo wa kuhiji. Muislamu mwenye wasaa ni vyema amlipie gharama nduguye Muislamu kuteketeleza nguzo hii kuliko yeye kuikariri. Pia itasaidia kupunguza huko

⁷ Ahmad, Abu Daawud, Ibn Maajah, akaipa daraja ya 'Hasan' Al-Albaaniy katika Swahiyh-Ibn Maajah.

⁸ Ahmad, na kaipa daraja ya 'Hasan' Al-Albaaniy katika Irwaaul-Ghaliyl.

Makkah zahma zinazozidi kila mwaka na kusababisha ugumu wa kutekeleza 'ibaadah/nguzo hii.